# TAARIFA YA AWALI
## Uhuru wa kimsingi uliheshimiwa katika uchaguzi mkuu wa Kenya, lakini vipengele vya utaratibu vinahitaji kuboreshwa

**Kenya, Tarehe 11 Agosti 2022**

*Taarifa hii ya awali ya ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi wa EU (EU EOM) inatolewa kabla ya kukamilika kwa mchakato mzima wa uchaguzi. Hatua muhimu zimesalia, ikiwemo uwasilishaji wa matokeo na uamuzi wa maombi kwenye mahakama. EU EOM kwa sasa iko katika nafasi ya kutoa maoni tu kuhusu uchunguzi uliofanywa hadi sasa, na baadaye itachapisha ripoti ya mwisho ikijumuisha uchambuzi kamili na mapendekezo kuhusu mageuzi ya uchaguzi. EU EOM pia inaweza kutoa taarifa za ziada kuhusu masuala yanayohusiana na uchaguzi pale inapoona inafaa.*

## Muhtasari

Wapiga kura nchini Kenya walielekea vituoni Agosti 9 2022 na kupiga kura zao kwa uvumilivu katika viwango sita vya uchaguzi. Haki za kimsingi ziliheshimiwa wakati wote wa kampeni lakini mabadiliko katika dakika za mwisho za mchakato wa uchaguzi ulionesha kuwa kuwa kuna mambo yanayostahili kuboreshwa. Wakati wa siku ya kupiga kura, kufunguliwa, upigaji kura na kuhesabiwa vilifanywa kuambatana na mipangilio iliyowekwa lakini hatua muhimu za uadilifu zilikiukwa hasa wakati wa kuhesabiwa kura ambao unahitaji utekelezwaji bora. EU EOM inaelewa kuwa ujumuishaji wa kura bado unaendelea na waangalizi wake wanaendelea kuangalia hadi mchakato wote wa uchaguzi utakapokamilika.

Kipindi cha uchaguzi kilipokaribia, kulikuwa na mvutano mdogo kuliko ilivyokuwa hapo awali. Vyama na wagombea waliweza kufanya kampeni kwa uwazi kote nchini ili kufikisha ujumbe wao kwa wapiga kura na uhuru wa kukusanyika ukaheshimiwa. Ijapokuwa uchaguzi wa urais ulikuwa na umuhimu wa juu zaidi, umuhimu wa kinyang'anyiro cha uchaguzi wa ugavana ulisisitiza ukuaji wa mamlaka ya ugatuzi tangu mwaka wa 2013.Vile vile, mbinu ya kupunguza na kutatua migogoro imeundwa ili kukabiliana na uwezekano wa kutokea migogoro. Hii ilisaidiwa na mjadala mpya wa kisiasa unaozingatia masuala ya kijamii na kiuchumi katika kampeni, ingawa mgawanyiko wa kikabila bado ulionekana. Lakini kulikuwa na kutojali sana, hasa kwa upande wa wapiga kura vijana.

Mojawapo ya masuala yaliyojitokeza sana katika chaguzi hizi ni ukosefu wa usimamizi mzuri wa fedha za kampeni ambao uliharibu mazingira ya kampeni. Hili lilisababisha kuwepo uwanja usio na usawa, na kuwanyima fursa wale walio na uwezo mdogo wa kifedha, haswa wanawake. Usambazaji mkubwa wa fedha uliofanywa na wagombea wengi kwa wapiga kura wakati wa kampeni ni kinyume na ahadi ya kuzingatia uchaguzi wa kidemokrasia na una ushawishi wa rushwa. Hatua ya bunge ya kupinga uundaji wa sheria za kudhibiti fedha za kampeni kabla ya uchaguzi, inasisitiza haja ya dhamira ya kweli ya kisiasa na utekelezaji. Ingawa awali uchaguzi ulisimamiwa kwa njia inayofaa na ya kitaalamu na tume huru ya uchaguzi na mipaka IEBC, hasa mchakato ulipoanza, siku ya uchaguzi ilipokaribia, hali ya sintofahamu nyingi iliendelea, na

kuathiri utaratibu wa siku ya uchaguzi. Mashaka haya yalitokana na IEBC kutaka kujibu ukosoaji wa hapo awali, mara nyingi kwenda zaidi kuliko ilivyoainishwa na sheria. Mengi ya maamuzi haya yangeweza kuzingatiwa mapema lakini badala yake yalishughulikiwa punde yalipotokea. Vilevile, IEBC ingeweza kufanya zaidi kwa kuwasiliana kwa uwazi zaidi na washikadau katika mchakato mzima ili kuboresha uaminifu wa umma, hata hivyo hili liliboreshwa katika wiki za mwisho.

Usajili wa wagombea uliwaandikisha watu 16,098 kwa chaguzi zote 6, na kuwapa wapiga kura chaguo la kweli. Ni wanawake 1,962 tu (asilimia 12) waliogombea, chini ya ilivyotarajiwa kulingana na juhudi za kikatiba kutoka kwa wadau wengi kuongeza ushiriki wao. Idadi ndogo ya maamuzi yalipingwa, ambayo yalishughulikiwa kwa haraka. (IEBC), hata hivyo, ilihitaji kusubiri maamuzi haya ili kukamilisha michakato fulani muhimu, kwa mfano, uchapishaji wa makaratasi ya kupigia kura. Mfumo wa kisheria unatoa msingi mzuri wa uendeshaji wa chaguzi za kidemokrasia na kwa jumla kuna kiwango cha juu cha imani ya umma kwa mahakama. Ingawa mipango ya kurekebisha vipengele vya sheria ya uchaguzi ikiwemo kutoka kwa IEBC, iliwasilishwa mara kwa mara kabla ya uchaguzi, na ilikwama bungeni, Sheria ya vyama vya kisiasa tu ndiyo ilifanyiwa marekebisho.

Utumiaji wa teknolojia katika uchaguzi huu ulikuwa suala kuu la mdahalo wakati wote wa mchakato wa uchaguzi, kutoka kwa ununuzi wake hadi kwa matumizi yake. Ijapokuwa IEBC ilisisitiza kwamba mchakato wa kutumia karatasi ulisalia kuwa msingi wa mfumo na kwamba mchakato wa kujumlisha matokeo unaweza kujengwa upya endapo mfumo utafeli, hii haikuwasilishwa ipasavyo kwa umma.

Katika muktadha wa sheria inayolinda uhuru wa kujieleza, vyombo vya habari viliangazia uchaguzi kwa upana kwa kutangaza redioni na televisheni na kuchapisha magazetini. Licha ya hali hii huru, waandishi wengi wa habari waliendelea kueleza wasiwasi wao kuhusu hatari na vitisho kwa taaluma yao katika kuripoti masuala nyeti, hasa kuhusu siasa na ufisadi. Mijadala ya wagombea, ambayo yalipeperushwa sana na vyombo vyote vya habari, ilikuwa fursa iliyokosa katika ngazi ya urais wakati wagombea wawili kati ya wanne walijiondoa.

Kutokana na ufuatiliaji wa vyombo vya habari vya EU EOM, ilibainika kuwa uchaguzi wa urais ndio uliangaziwa kwa kiwango kikubwa, ukifuatiwa na ule wa ugavana. Kituo cha habari cha serikali kiliwapa watu habari kwa upana. Mgombea mmoja wa urais alipewa muda mwingi katika vituo vya kibinafsi hasa kutokana na mjadala. Radio za lugha za asili zilionyesha upendeleo huku magazeti yakionyesha uwepo wa usawa kwenye habari walizochapisha.

Mitandao ya kijamii ilitumika sana wakati wote wa kampeni. Taarifa potofu zilienezwa kupitia mitandao, kukiwa na vipengele vya tabia isiyo ya kweli iliyoratibiwa iliyopatikana na kitengo cha ufuatiliaji wa mitandao ya kijamii cha EU EOM. Akaunti zilizo chini ya utambulisho wa uwongo zilitumiwa kusambaza ujumbe wa kupotosha.

Wapiga kura walitekeleza haki yao ya kupiga kura kwa njia ya amani siku yote ya uchaguzi. Shughuli ilikuwa yenye utulivu licha ya kuongezwa muda kutokana na mabadiliao yaliyofanwa yakiwa yamechelewa. Vituo vya kupigia kura vilivyotembelewa na waangalizi wa EU EOM

vilifunguliwa vikiwa vimechelewa katika sehemu nyingi kutokana haswa na kutokuwa tayari kwa wafanya kazi na hitilafu ya mitambo na kwa jumla ufumbuzi ulitathminiwa kuwa mbaya kautokana na idadi ya visa hivyo vingi. Wakati wa kupiga kura vifaa ya kielektroniki wakati mwingine vilikumbwa na hitilafu, na kusababisha kuongezeka kwa foleni. Kwa jumla waangalizi wa EU EOM waliridhishwa na zoezi la upigaji kura katika sehemu nyingi. Wakati wa kufungwa baadhi ya vituo vya kupigia kura havikufuata mchakato fulani ya kiusalama. Hata hivyo hakukuwepo na malalamiko yoyote yaliyoripotiwa kwenye vituo vilivyotembelewa. Ujumuishaji wa kura unaendelea lakini baadhi ya waangalizi waliripoti kuzuiliwa kushuhudia shughuli hiyo hali ambayo iliathiri uwazi.

*Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Ulaya (EU EOM) umekuwepo nchini Kenya tangu tarehe 27 Juni mwaka 2022 kufuatia mwaliko kutoka kwa mamlaka ya Kenya. Ujumbe huo unaongozwa na Mwangalizi Mkuu, Ivan Štefanec, Mbunge wa Bunge la Ulaya (Slovakia). Kwa jumla, EU EOM ilituma waangalizi 182 kutoka mataifa 30 Wanachama wa Umoja wa Ulaya, Pamoja na Kanada, Norway, na Uswizi kote nchini kutathmini mchakato mzima wa uchaguzi kulingana ahadi za kimataifa za uchaguzi wa kidemokrasia pamoja na sheria za nchini Kenya. Katika kipindi cha misheni hii, EU EOM imekutana na Zaidi ya washikadau 2562 wakiwemo mamlaka za serikali na mamlaka huru, wajumbe wa mahakama, vyama vya kisiasa na wagombeaji, asasi za kiraia, na wawakilishi kutoka kwenye vyombo vya Habari.*

*Ujumbe wa Bunge la Ulaya, unaoongozwa na Evin Incir, mbunge kutoka taifa la Sweden, pia ulijiunga na misheni na kuidhinisha Taarifa hii kikamilifu. Siku ya uchaguzi, waangalizi walitembelea vituo 750 vya kupigia kura katika kaunti 39 kati ya 47 ili kuangalia upigaji kura kuhesabu na kujumlisha.*

*Taarifa hii ya awali inatolewa kabla ya kukamilika kwa mchakato wa uchaguzi. Tathmini ya mwisho ya uchaguzi itategemea, kwa kiasi fulani, hatua zilizosalia za mchakato wa uchaguzi, hasa, kujumlisha matokeo, na kushughulikia malalamiko na rufaa zinazoweza kuibuka baada ya siku ya uchaguzi.*

*EU EOM itasalia nchini kuangalia yatakayojiri baada ya uchaguzi na itachapisha ripoti ya mwisho, yenye mapendekezo ya kina, ndani ya miezi miwili baada ya kukamilika kwa mchakato wa uchaguzi.*

## TAARIFA YA AWALI

Tarehe 9 Agosti 2022, Kenya ilifanya uchaguzi mkuu wa tatu chini ya Katiba ya mwaka 2010, ikipiga kura katika chaguzi sita tofauti. Kinyang’anyiro cha urais hutumia mfumo wa walio wengi (zaidi ya asilimia 50), huku kukihitajika angalau asilimia 25 ya kura katika kaunti 24 kati ya 47. Chaguzi nyingine tano ni: uchaguzi wa magavana 47 wa kaunti, wabunge 290 wa Bunge la Kitaifa , wanawake 47 katika Bunge la Kitaifa, maseneta 47, na wabunge 1450 wa kaunti (MCA). Zaidi ya hayo, wanachama wanaowakilisha wanawake, watu wenye ulemavu, vijana, wafanyakazi, na walio wachache hupendekezwa na vyama sawia na mgao wao wa kura katika bunge na mabunge ya kaunti.

Kulikuwa na mzozo kati ya Rais Kenyatta na Naibu wake Ruto ambao ulisababisha mvutano ndani ya tabaka la kisiasa lakini haukuleta mvutano mkubwa wa kikabila. Asili ya kikabila ya miungano yote miwili, Azimio la Umoja ya Odinga yenye vyama 23 chini ya mwavuli wake na Kenya Kwanza ya Ruto yenye vyama 12, ilisuluhisha mvutano mkali.

Nafasi za uchaguzi katika ngazi ya kaunti zimewavutia zaidi wapiga kura kwa kuwa wametambua kwamba maendeleo hayategemei urais pekee; hili limepunguza mivutano. Muundo thabiti wa usalama wa serikali, uliowekwa katika katiba ya 2010 na ulioendelezwa kutokana ya msingi wa ghasia za baada ya uchaguzi uliopita, unaongezewa na mipango mbalimbali, isiyo ya serikali. Hii imeanzisha michakato ya amani ambayo hupunguza migawanyiko.

Licha ya mahakama kutambuliwa, heshima ya utawala wa sheria kutoka kwa serikali na wabunge kila wakati sio thabiti. Hii inaashiriwa na ukosefu wa nia ya kutekelezwa kwa maamuzi ya korti kuhusu sheria ya usawa wa kijinsia wa theluthi mbili kulingana na katiba. Inaashiriwa pia na ukosefu wa utekelezaji wa sheria ya mashirika ya manufaa ya umma ambayo imeyaweka mashirika ya asasi za kiraia katika hatari ya kuingiliwa na serikali kiholela.

Changamoto iliyoibuka kabla ya uchaguzi mkuu ilitokana na kuzorota kwa uchumi, kuongezeka kwa hatarishi ya kijamii, na kwa viwango vya umaskini kwa wananchi wengi. Hii ilisababisha kupanda kwa bei ya mafuta, bidhaa muhimu za chakula, na bidhaa za kilimo kutokana na janga la COVID-19 na vita nchini Ukraine.

## Mfumo wa Kisheria na Uchaguzi

Mfumo wa kisheria unatoa msingi mzuri wa uendeshaji wa chaguzi za kidemokrasia. Kenya ni mshirika wa vyombo vingi vya kisheria vya kikanda na kimataifa, ambavyo vinaweka ahadi za utawala wa sheria na uchaguzi wa kidemokrasia.

Katiba ya Kenya mwaka 2010, ni chombo cha mabadiliko ambacho huweka haki nyingi za ushiriki wa kisiasa. Masharti ya hatua ya uthibitisho yanakuza wanawake, watu wenye ulemavu, vijana, na walio wachache katika ofisi zilizochaguliwa kupitia hatua mbalimbali. Hata hivyo, mabunge yaliyofuatana yameshindwa kuwasilisha sheria inayohitajika kutekeleza masharti haya, na kuacha hatua hii kwa kutotimizwa kwa kiasi kikubwa.

Ulinzi hutolewa kwa utekelezaji wa haki za kisiasa, ikiwa ni pamoja na haki ya kupiga kura na kugombea uchaguzi, pamoja na uhuru wa kujumuika, kukusanyika na kujieleza. Haki za kupiga kura na kugombea ziko chini ya vikwazo, na vizuizi vimewekwa: na ambayo ni wazi kabla ya hatua zozote za mahakama kufanyika, ambavyo ni kinyume cha ahadi za kimataifa. Kutofautiana katika chaguzi zote sita, hizi ni pamoja na vizuizi kwa msingi wa uwezo wa kiakili, kufilisika, kutokuwa na digrii na kushindwa kukidhi masharti magumu ya uraia na ukaazi.

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, 2022, na seti iliyofuata ya rasimu tano za Kanuni za Uchaguzi, 2022, ambazo zingeleta uwazi katika vipengele vingi muhimu vya kiutaratibu, hazikupitishwa na bunge, licha ya kuhimizwa na IEBC. Bunge pia lilizuia kuidhinishwa kwa kanuni za fedha za kampeni, na kuacha matumizi yasiyodhibitiwa. Kutungwa kwa Sheria ya Kulinda Data, 2019, na Sheria ya Vyama vya Kisiasa (Marekebisho) ya 2022,

kuliwakilisha baadhi ya hatua chanya za mageuzi ya sheria, huku sheria hiyo ikiwa imechangia katika michakato ya amani zaidi ya uteuzi wa vyama vya kisiasa.

Ufikiaji wa umma kwa nakala za kisheria ni mzuri, kama vile ufikiaji wa suluhisho la kisheria. Sheria na maamuzi ya mahakama yanapatikana mtandaoni, huku janga la COVID-19 likiharakisha uhamishaji wa kesi mtandaoni, huku kesi zikiwasilishwa kwa njia ya kielektroniki na kusikilizwa kupitia mtandao. Sheria zilizopo kulinda haki za kikatiba ziko wazi, na zinaruhusu utetezi wa mara kwa mara wa haki za kisiasa.

### Usimamizi wa Uchaguzi

Hapo awali IEBC iliendesha uchaguzi kwa ufasaha, ikitimiza makataa yote ya kisheria, lakini siku ya uchaguzi ilipokaribia, ukosefu wa uhakika katika masuala kadhaa muhimu uliongezeka ambao uliathiri shughli za siku ya uchaguzi. Hali hii ulitokana na IEBC kutaka kujibu malalamiko ya awali. Mengi ya maamuzi haya yangeweza kuzingatiwa mapema lakini badala yake yalishughulikiwa punde yalipoibuka. Pia kulikuwa na wasiwasi kutokana na kesi za mara kwa mara. Vilevile, IEBC ingeweza kufanya zaidi kwa kuwasiliana kwa uwazi zaidi na washikadau katika mchakato mzima ili kuboresha uaminifu wa umma, hata hivyo hili liliboreshwa katika wiki za mwisho.

Uajiri uliogatuliwa wa wanachama wa vituo vya kupigia kura ulifanyika kwa uwazi na kwa ushindani. Mfumo wa kupokezana wasimamizi wa uchaguzi wa kaunti na maeneo bunge kabla ya uchaguzi unatambuliwa na wadau wa uchaguzi kuhakikisha kutopendelea kwenye mamlaka ya uchaguzi katika ngazi za chini huku ajira ya kudumu kwao unchangia uwepo wa uzoefu wa kazi. IEBC ilionyesha umahiri katika utoaji wa mafunzo.

Hata hivyo, ucheleweshaji wa usambazaji wa fedha kwa ajili ya elimu ya wapigakura ulichelewesha kuanza kwa shughuli na kuathiri vibaya uwezo wa wafanyikazi wa IEBC mashinani, ambao walikuwa na usaidizi mdogo wa vifaa.

Badala ya kufuata sheria na kupunguza utumizi mbaya wa rejista iliyochapishwa, IEBC iliamua kuchapisha rejista za wapigakura katika bahasha salama na kuzitumia tu iwapo Mfumo wa Kieletroniki (KIEMS) utafeli kabisa. Uamuzi huu ulizua utata miongoni mwa washikadau wa uchaguzi na pia ulipingwa mahakamani, na kusababisha IEBC kubatilisha msimamo wao wa awali na kuanzisha tena matumizi ya sajili iliyochapishwa ya wapigakura siku ya uchaguzi. Ikilenga kuzuia udanganyifu katika uchaguzi, IEBC pia ilianzisha ulinzi wa ziada wa kuwatambua wapigakura. Licha ya hayo, matumizi ya KIEMS kwa utambuzi wa wapigakura na uwasilishaji wa matokeo yalisalia kuwa suala la wasiwasi kwa waangalizi wote wa EU EOM, ingawa IEBC ilikariri imani yake katika utendakazi bora wa mfumo huo.

EU EOM inabainisha kuwa IEBC imechukua hatua fulani, ikiongozwa na uamuzi wa Mahakama ya Juu wa 2017, kurekebisha uwasilishaji wa matokeo ya uchaguzi wa urais katika kituo cha kupigia kura, ambayo yamesalia kwenye karatasi, na ilihitaji picha za fomu (34A) pekee kutumwa badala ya kuzituma pamoja na uandikishaji wa matokeo wa KIEMS. Uamuzi huu, pamoja na ushahidi wa karatasi, ulibainiwa na waangalizi wengi wa EU EOM kama hatua ya

kuimarisha uadilifu. EU EOM inabainisha kuwa kuachana na uwekaji data wa moja kwa moja katika KIEMS katika ngazi ya kituo cha kupigia kura huchangia katika uthibitishaji na uwazi wa mchakato huo. Kwa kuzingatia kanuni hizo, IEBC pia ilichukua hatua kukabiliana na ukosefu wa mtandao wa 3G/4G katika vituo 1,272 vya kupigia kura kote nchini kupitia utumizi wa modemu za satelaiti za uwasilishaji wa matokeo.

## Teknolojia ya Uchaguzi

Uchaguzi ulitumia mfumo jumuishi wa kielektroniki wenye usajili wa wapiga kura kwa njia ya kielektroniki, utambulisho wa kielektroniki wa wapigakura na uwasilishaji wa matokeo kielektroniki. IEBC iliendesha michakato kadhaa ya ununuzi wa umma, ikijumuisha ya mfumo wa KIEMS na mtandao wake, na ukaguzi wake, kama inavyotakiwa na sheria na kanuni. Hata hivyo, utathmini wa mchakato wa ununuzi wa KIEMS haukuwekwa wazi, hivyo kudhoofisha uwazi.

Utendaji kazi wa mfumo mpya wa KIEMS ulitatizwa kwa sababu ya usimamizi duni na ukosefu wa uratibu kati ya taasisi. Utoaji wa kandarasi uliochelewa, ugumu wa kutumia tena vifaa vya KIEMS na data ya zamani ya usajili wa wapigakura, pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara ya mahitaji kutokana na kutokuwa na uhakika wa kisheria yaliibua wasiwasi wa washikadau kuhusu utayari wa mfumo huo. Ingawa IEBC ilifanya majaribio ya uwasilishaji wa matokeo mara mbili, ulikuwa mdogo kwa kiwango na upeo, haukuondoa kikamilifu shaka juu ya ufanisi na kutegemewa kwa mfumo huo. Kukamatwa kwa wafanyikazi wanakandarasi na jinsi suala hilo lilivyo shughulikiwa pia kunaweza kudhoofisha imani ya umma.

Upeo wa ukaguzi wa teknolojia ya uchaguzi ulihusisha kukubalika kwa mfumo wa KIEMS, na usalama, na ubora wa vituo vya data vya IEBC kupokea na kuchakata matokeo ya uchaguzi. Vilevile, ukosefu wa taarifa za umma kuhusu matokeo ya ukaguzi wa mfumo na uboreshaji uliotekelezwa ulipunguza mchango wake katika kuboresha imani katika teknolojia ya uchaguzi. Ingawa ukaguzi haufanywi kikamilifu kwa umma, kwa sababu za kiusalama zinazoeleweka, hitaji la kiwango fulani cha habari kwa washikadau ni muhimu ili kujenga imani ya umma.

## Usajili wa Wapiga Kura

Tume ya IEBC ilifanya zoezi lililoboreshwa la awamu mbili la usajili wa wapigakura, likilenga wapigakura wapya milioni 6. Ingawa haijafikia lengo lake, asilimia 74.82 ya wananchi walio na vitambulisho vya kitaifa wamejumuishwa katika daftari la mwisho la wapigakura. Pengo la usajili lilichangiwa zaidi na kutojali kwa vijana, pamoja na uhamasishaji usio wa kutosha wa IEBC kabla ya zoezi hilo, uliosababishwa na mapungufu ya ufadhili. Waangalizi wa EU EOM hawakuibua mashaka makubwa juu ya ujumuishaji kwenye mchakato au ubora wa rejista ya wapiga kura. Hata hivyo, uhamisho wa wapiga kura uliochochewa kisiasa ulitajwa kwa waangalizi wa Umoja wa Ulaya katika baadhi ya maeneo, huku IEBC yenyewe ikifanya uchunguzi kuhusu uhamisho haramu wa wapiga kura katika kaunti mbili. Ingawa matokeo ya jumla ya ukaguzi wa KPMG yalitolewa na IEBC tarehe 20 Juni, ripoti halisi iliwekwa wazi wiki moja tu kabla ya uchaguzi, jambo ambalo liliathiri vibaya uwazi wa mchakato huo, ingawa IEBC ilidaiwa kushughulikia mapungufu.

Wapiga kura wangeweza kuangalia data zao za usajili kwa SMS, lakini kwa kuwa hii ilihusisha ada ya shilingi 10 za Kenya, haikutumiwa sana. Sehemu kwenye tovuti ya IEBC ambayo pia iliruhusu wapiga kura kuangalia taarifa zao za usajili kwa bahati mbaya haikuweza kupatikana kwa wakazi wengi wasiokuwa na mtandao. Lakini, wapiga kura walipewa muda wa siku 30 kwa uthibitishaji kwenye vituo vya IEBC. Daftari la mwisho la wapiga kura lililotangazwa kwenye gazeti la serikali tarehe 21 Juni 2022 lilikuwa na jumla ya wapiga kura 22, 120,458. Wanawake walichangia asilimia 49.12 na watu wenye ulemavu kwa asilimia 18.94.

## Usajili wa Wagombea na Vyama vya Siasa

EU EOM ilitathmini mchakato wa usajili wa wagombea kama unaotoa chaguo pana la kisiasa. Tume ya IEBC iliidhinisha vyama 83 kati ya 89 vilivyosajiliwa kushiriki uchaguzi huo. Kukiwa na mashindano sita tofauti ya uchaguzi, wagombea 16,098 (ikiwa ni pamoja na wanawake 1,962, kama ilivyoripotiwa na IEBC) walisajiliwa katika ngazi zote. Usajili wa vyama vya siasa unadhibitiwa sana na unasimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Katiba inampa kila raia haki ya kugombea uchaguzi, huku sheria ikipeana usajili wa vyama vya siasa na wagombea binafsi. Watu wenye "matatizo ya akili" wamekataliwa, kinyume na Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.

IEBC ilifanya juhudi kubwa kutekeleza kanuni ya thuluthi mbili ya jinsia katika usajili wa orodha ya vyama, huku asilimia 98 ya vyama vikitii. Utekelezwaji wake hata hivyo ulitupiliwa mbali na mahakama Juni 13 kwa misingi ya, *miongoni mwa mambo mengine*, kutoshirikishwa kwa umma. IEBC pia ilisisitiza kuhakikisha kuwa orodha za vyama vya kisiasa zinazingatia sheria za uwakilishi wa makundi maalum.

## Mazingira ya Kampeni

Waangalizi wa EU EOM waliona kwamba washiriki waliweza kufanya kampeni kwa uwazi kote nchini ili kufikisha ujumbe wao kwa wapiga kura na kwamba uhuru wa kimsingi wa kukusanyika uliheshimiwa. Muundo wa makabila mbalimbali ya miungano miwili mipana ilisaidia kupunguza mivutano baina ya makabila katika muda wote wa kampeni. Hakuna matukio ya matumizi ya nguvu kupita kiasi na polisi yaliripotiwa, na hakuna kesi za lugha za uchochezi zilitambuliwa na EU EOM katika shughuli za kampeni. Wadadisi kadhaa waliangazia hali ya vitisho dhidi ya wagombea wanawake katika maeneo mengi. Pia kutoridhishwa kwa vijana kulishuhudiwa.

Uchaguzi huo ulikuwa na sifa ya wagombea wote wawili kufurahia mambo ya uongozi na upinzani. Mgombea wa Kenya Kwanza, William Ruto, alikuwa naibu rais. Mgombea wa Azimio la Umoja, Raila Odinga, aliidhinishwa na Rais Kenyatta. Wakati huo huo, Ruto alikuwa amepoteza baadhi ya mamlaka yake kutokana na kutofautiana kwake na rais, na Odinga amekuwa kiongozi wa upinzani kwa miongo mingi. George Wajackoyah (Roots Party) na David Waihiga (Agano Party) pia walishindana.

Kampeni zilijikita katika masuala ya kijamii na kiuchumi, huku ukabila ukionekana kutumiwa. Ruto aliendesha kampeni yake kama kinyang'anyiro kati ya enzi kuu za kisiasa zilizokita kati ya

wanasiasa wa zamani na yeye mwenyewe na mgombea mwenza, Rigathi Gachagua, kama wanasiasa walioibuka wenyewe kutoka chini hadi nyadhifa za uongozi wa kitaifa. Odinga alisisitiza sifa zake na za mgombea mwenza wake (Martha Karua) katika mapambano yao ya mfumo wa vyama vingi, vita vyao dhidi ya ufisadi, na tajriba yake ya awali kama waziri mkuu. Kampeni za Odinga zilibanwa kwa kiasi fulani na muungano wake na Rais Kenyatta, kushindwa kujitenga na sera za serikali. Wagombea wote wawili walisisitiza uchumi, lakini Ruto alisisitiza mfumo wa 'chini juu'.

Wagombea walifanya kampeni kwa njia mbalimbali. Mikutano ya urais kote nchini kwa kawaida ilikuwa mikubwa, ikivutia umati mkubwa. Mara nyingi, baada ya mgombea mmoja wa urais kutembelea mkoa, mwingine alifuata ndani ya siku moja au mbili. Wagombea wote wakuu wa urais mara nyingi waliandamana na wagombea wa ndani wa muungano wao, wakitaka kuidhinishwa. Hili, wakati fulani, lilizua ushindani mkali na hali ya wasiwasi ndani ya vyama vya muungano zikaibuka katika maeneo kadhaa.

Umuhimu wa kinyang'anyiro cha ugavana katika chaguzi hizi ulisisitiza umuhimu wa ugatuzi wa mamlaka kikatiba tangu 2013, na kuonyesha kuongezeka kwa ukomavu wa kisiasa. Takriban nusu ya viti vya ugavana vilikuwa wazi, huku viongozi waliokuwa madarakani wakihitimisha muhula wao wa pili na wa mwisho. Uchaguzi wa MCA pia ulivutia wapiga kura wengi. Ingawa wagombea wa ugavana pia walifanya mikutano mikubwa, kampeni za chaguzi zingine zilikuwa ndogo zaidi (misafara ya uchaguzi, mikutano ya nyumba kwa nyumba na mikutano ya ukumbi mijini).

Utoaji wa pesa taslimu kutoka kwa wengi wa wagombea kwa wapiga kura wakati wa kampeni ni kinyume na uchaguzi wa kidemokrasia na ina ushawishi wa ufisadi. Kutokana na kukosekana kwa kanuni za fedha za kampeni, wagombea walitumia kiasi kikubwa cha fedha katika utoaji wa hongo moja kwa moja kwa waandaaji, wafuasi na wahudhuria mikutano. Hili lilishuhudiwa na EU EOM katika visa 21 na kuripotiwa na waangalizi wengi katika ngazi ya kitaifa na kaunti.

Ukiukaji wa udhibiti wa kampeni, kama vile matumizi mabaya ya mamlaka ulibainishwa na waangalizi wa EU EOM katika visa kadhaa ambavyo pia viliripotiwa na vyombo vya habari. Waangalizi wa EU EOM pia walipokea baadhi ya ripoti kwamba mawaziri na makatibu wakuu machifu na Wasaidizi wa machifu walimpigia kampeni mgombeaji urais wa Azimio kule mashinani kinyume na sheria ya kutopendelea upande wowote kwa maafisa wa serikali. Matumizi ya mamlaka ya magavana katika kaunti kadhaa zinazopendelea Kenya Kwanza pia yalibainishwa. Siku moja baada ya kumalizika kwa kampeni, Rais Kenyatta alifanya mahojiano ya runinga/redio kwa lugha ya Kikuyu, akiwaomba wapiga kura wa eneo la Mlima Kenya kuungana, akiweka wazi kwamba wanapaswa kumpigia kura Odinga.

Madai ya ufisadi dhidi ya Ruto na Gachagua kutoka kampeni ya Azimio na kujibu madai hayo kupitia “kulishika taifa” kupitia Kenyatta, Odinga na wadhamini wao yaliyotolewa na timu ya Kenya Kwanza yalitawala wiki za mwisho za kampeni. Gachagua, akiwa na mashtaka mawili ya ufisadi dhidi yake, aliamriwa na Mahakama Kuu mwishoni mwa Julai 2022 kusalimisha shilingi milioni 200 za Kenya, ambazo alikuwa ameshindwa kujibu chanzo chake. Wiki zilizopita za

kampeni pia zilishuhudia mabishano makali na ya kibinafsi kati ya Ruto na Kenyatta juu ya mzozo wao ambao ulizidisha mvutano kati ya kambi hizo mbili.

## Vyombo vya habari

Mfumo wa kisheria unatoa nafasi ya kutosha ya uhuru wa kujieleza. Hata hivyo, wanahabari wengi wa kuaminika kote nchini walioripoti kwa EU EOM wanaonyesha kuwa waandishi wa habari wanaendelea kutishwa wanapoandika maswala ya kisiasa na ufisadi. Waandishi wa habari walielezea wasiwasi kuhusu usalama wao walipokuwa wakiripoti kuhusu baadhi ya mikutano ya kampeni.

Kwa ujumla, vyombo vya habari viliripoti kwa upana uchaguzi, kwa kuzingatia kinyang'anyiro cha urais, kuwapa wapiga kura kiwango cha kutosha cha habari ambacho wangetegemea kufanya chaguo lao. Vyombo vya habari vilitenga programu na sehemu maalum kwa uchaguzi, na vyombo vya habari vya kielektroniki viliandaa mijadala katika ugavana, wawakilishi wa wanawake, bunge la kitaifa na ngazi ya useneta.

Ingawa kuna uhuru wa vyombo vya habari, ni vyombo vya habari vichache pekee vilivyo na uhusiano wa kisiasa na kibiashara vinadhibiti vikundi vya habari vyenye ushawishi mkubwa. Miongozo ya ushughulikiaji wa uchaguzi iliwekwa wazi ambayo inasisitiza kutopendelea na usawa kama kanuni muhimu. Hata hivyo, baadhi ya wamiliki wa vyombo vya habari waliunga mkono hadharani kambi ya Azimio, ambayo inaweza kuwa imechangia madai ya upendeleo wa waandishi wa habari kwa wafanyakazi wake.

Kujiondoa kwa wagombea wawili kwenye mdahalo wa urais kulifanya kuwa na uwakilishi mdogo. Kwa kuzingatia muundo wa 2+2 uliokusudiwa awali, wawili waliosalia, Ruto na Waihiga, walijibu maswali tofauti, badala ya mjadala. Lakini iliwapa wananchi fursa ya kutathmini utendaji wa baadhi ya wagombea na uhakiki ulifanywa na waandaaji na vyombo vya habari kuhusu taarifa za wagombea. Wakati wa uwasilishaji wa Ruto, kupotea nguvu za umeme kuliripotiwa sehemu mbalimbali za nchi, kama ilivyothibitishwa na waangalizi wa EU EOM. Kampuni ya kitaifa ya umeme iliomba msamaha rasmi kwenye tovuti yake, lakini waangalizi wengi waliiona kuwa ilikuwa ni ya kisiasa.

Ufuatiliaji wa vyombo vya habari wa EU EOM uligundua kuwa shirika la utangazaji linalomilikiwa na serikali lilitenga muda wa bure wa maongezi kwa vyama vya siasa na wagombea wakati wa kampeni, ingawa hakuna vigezo vya mgao wa nafasi vilivyowekwa. Vituo vya runinga vya kibinafsi vilitoa muda zaidi wa hewani kwa mgombeaji wa Kenya Kwanza Ruto, haswa kutokana na mjadala huo.

Redio inasalia kuwa chanzo kikuu cha habari kwa wapiga kura wengi. Vituo vya redio vya lugha za asili vilionyesha upendeleo kwa kambi moja au nyingine kuu katika suala la utangazaji. Hili lilibainika zaidi kwenye Ramogi FM, redio ya jamii ya Wajaluo, ambayo ilimpigia debe mgombea urais wa Azimio kulingana na wakati, na Kass FM, redio ya jamii ya Wakalenjin, kwa kutenga muda na sauti chanya kwa mgombeaji wa Kenya Kwanza. Magazeti yalitoa habari zenye uwiano zaidi.

Kinyang'anyiro cha ugavana kilikuwa uchaguzi wa pili ulioangaziwa zaidi. Televisheni na magazeti yaliwagawia wagombeaji wa UDA na Jubilee sehemu kubwa ya matangazo, huku katika vituo vya redio vilivyofuatiliwa na EU EOM, wagombeaji wa ODM walitawala.

Idadi ya matangazo ya televisheni kutoka kwa wagombea wote wawili wa nafasi za urais iliongezeka mara tatu katika wiki ya mwisho ya kampeni, huku muda wa televisheni unaolipwa mara kwa mara kupitia kampeni ulitoka kwa wagombea wa UDA. Matangazo ya kisiasa katika vituo vya redio na magazeti yaliangazia zaidi muungano wa Azimio.

## Mitandao ya kijamii

Vyama na wagombeaji walitumia majukwaa ya mitandao kufanya kampeni, kuanzisha tovuti, kuajiri wanablogu na washawishi, pamoja na wasimamizi wa kampeni za kidijitali kudhibiti akaunti zao. TikTok iliibuka kama moja ya programu maarufu ya mtandao katika kampeni

CSOs zilifanya jitihada za kweli kufuatilia mitandao ya kijamii ili kukabiliana na taarifa potofu na kuongeza uelewa wa matumizi mabaya ya majukwaa ya mtandaoni na watendaji wenye nia mbaya kueneza 'matamshi ya chuki', katika kipindi cha kuelekea uchaguzi. Meta, Twitter na TikTok zilitangaza hatua mahususi ili kusaidia kuhakikisha nafasi salama ya kidijitali na kutoa taarifa za wapigakura wakati wa mchakato wa uchaguzi. Licha ya hayo, majukwaa yote yalitumiwa vibaya kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendakazi wa kupotosha taarifa, kwa kutumia mbinu nyingi kuchochea uhaba wa habari kupitia kampeni za udanganyifu na mashambulizi ya kibinafsi, ikilenga IEBC, mahakama, vyombo vya habari na wanasiasa. Wagombea wanawake pia walikuwa wahasiriwa wa unyanyasaji kwenye mitandao ya kijamii.

Kuchelewa kwa TikTok kushughulikia ukiukaji wa sera zake kuhusu tabia ya chuki na taarifa potofu zenye madhara kuliwezesha kuenea kwa matamshi ya uchochezi kuhusu uchaguzi kwenye jukwaa kupitia vitisho vya ghasia za kikabila zinazolenga wanajamii fulani. EU EOM ilitambua maudhui potofu ambayo yalitazamwa kwa wingi yakiwa na taarifa za uwongo, lugha ya uchochezi, vyombo vya habari vya uwongo vya dijitali. Maudhui yaliyoibua vurugu za zamani za uchaguzi nchini Kenya kwa manufaa ya kisiasa pia yalizingatiwa.

EU EOM ilitambua akaunti kadhaa za mitandao ya kijamii unaohusishwa na wagombea urais kwenye Facebook, Twitter, Instagram, TikTok na YouTube, kukiwa na visa vingi vya utumiaji wa picha za wasifu zinazofanana au kupotohswa kidogo. Kati ya hizi, zaidi ya akaunti 200 ziliundwa tangu Juni mosi. Wakati wa uchunguzi wa EU EOM, nyingi zilifungwa na kuondolewa, au kubadilisha majina yao kuwa masomo yasiyohusiana na uchaguzi. Maendeleo haya yanaunga mkono madai yaliyoenea ya watumiaji kulipwa ili kueneza jumbe za kampeni kupitia akaunti za mtandaoni chini ya utambulisho wa uongo ili kusambaza au kukuza simulizi katika chaguzi hizi. Licha ya kukiuka viwango vya jumuiya za majukwaa, akaunti nyingi kama hizo ziliendelea kutumika hadi siku ya uchaguzi.

Baraza la Mitandao ya Kijamii inayowajibika ilileta pamoja wawakilishi kutoka mashirika ya kiraia na watu mashuhuri siku chache kabla ya uchaguzi. Ilidai uwajibikaji bora kutoka kwa makampuni makubwa ya teknolojia nchini Kenya. Pia ilihimiza mamlaka kuunda na kutia saini

hadharani Kanuni ya Mazoezi ya kujidhibiti na habari potofu, kulingana na utendaji mzuri wa kimataifa.

**Mwananchi na Uangalizi wa Kimataifa**

Shirika kuu la waangalizi wa uchaguzi wa wananchi, Kundi la Waangalizi wa Uchaguzi (ELOG) lilipeleka waangalizi wa muda mrefu 290 nchi nzima, wakati wa siku ya uchaguzi walikuwa na waangalizi wa muda mfupi wapatao 5,108 na kufanya majumuisho ya kura sambamba (PVT) kwa kinyang'anyiro cha urais. Baraza la Maaskofu Katoliki Kenya pia lilituma waangalizi wapatao 1,800 siku ya uchaguzi, wakati shirika la Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana likipeleka karibu waangalizi 3,000. Taasisi nyingine, kama vile Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya, ilisambaza waangalizi kote nchini kufuata masuala ya haki za binadamu yanayohusiana na uchaguzi, huku Kitengo Huru cha Medico-Legal Unit kikifuatilia hali hiyo tangu Machi kikiwa na waangalizi 86.

Misheni kadhaa za waangalizi wa kimataifa zimetumwa kwa chaguzi hizi. Umoja wa Afrika pamoja na Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA), Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Taasisi ya Uchaguzi ya Demokrasia Endelevu Afrika (EISA), Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD). ), misheni ya pamoja ya Taasisi ya Kitaifa ya Kidemokrasia (NDI) / Taasisi ya Kimataifa ya Republican (IRI). Kituo cha Carter na Wakfu wa Westminster wa Demokrasia (WED) walituma misheni ya wataalam, wakizingatia vipengele mahususi. EU EOM ilishirikiana karibu na wote chini ya mfumo wa Azimio la Kanuni.

**Kupiga Kura, Kuhesabu na Kujumlisha**

Wapiga kura walitumia haki yao ya kidemokrasia ya kupiga kura kwa njia ya amani kwa ujumla siku nzima ya uchaguzi. Mchakato ulikuwa shwari, ingawa ulikuwa wa muda mrefu, na wafanyikazi waliojitolea wa vituo vya kupigia kura ambao walilazimika kukabiliana na mabadiliko ya dakika za mwisho katika vipengele muhimu vya utaratibu kutokana na amri ya mahakama ya rufaa.

Vituo vya kupigia kura vilivyotembelewa na waangalizi wa EU EOM vilifunguliwa kuchelewa katika kesi 28 kati ya 33, kutokana na kutojiandaa kwa wafanyikazi na vifaa vya kielektroniki (KIEMS) kutofanya kazi. Mawakala wa vyama walikuwepo katika vituo vyote vilivyotembelewa. Mwenendo wa jumla wa ufunguzi ulitathminiwa kuwa "mbaya" au "mbaya sana" katika vituo 4 kati ya 33 zilivyootembelewa, ikiwa ni idadi kubwa.

Wakati wa upigaji kura, utambuzi wa wapigakura wa kibayometriki ulikuwa na tatizo katika vituo 29 kati ya 430 vilivyotembelewa, huku KIEMS havikuweza kuthibitisha alama za vidole mara moja na kulazimika kuthibitisha alphabeti. Hii ilisababisha foleni ndefu. Vyema, wafanyakazi wa upigaji kura walifuata taratibu katika vituo 135 ya 151 ambapo suala hili lilizingatiwa. Utumizi usioendana wa kanuni za utumiaji wa daftari la wapiga kura lililochapishwa ulibainika katika idadi ndogo ya vituo vilivyotembelewa, kutokana na uamuzi wa

mahakama ya rufaa uliotolewa usiku wa kuamkia siku ya upigaji kura, kwa kuzingatia kwamba daftari lililochapishwa lilipaswa kutumika baada ya kufeli kwa vifaa vya kieletroniki.

Kukagua vidole vya wapiga kura kwa wino haukufanyika katika vituo 110 kati ya 430 vilivyotembelewa, ambayo ni ukiukaji muhimu wa utaratibu. Mpangilio wa vituo 88 kati ya 430 vilivyotembelewa haukufaa kwa watu wenye ulemavu. Taratibu zinazohusiana na upigaji kura wa kusaidiwa hazikufuatwa katika vituo 60 kati ya 144 ambapo upigaji kura wa kusaidiwa ulizingatiwa, wakati uwekaji wino wa kidole cha msaidizi haukufanyika katika ya 62 kati ya izi.

Usiri wa kura haukulindwa kikamilifu katika vituo 184 kati ya 430 vilivyoangaliwa, kwa sababu ya mpangilio wa vituo. Msongamano ulibainika katika vituo 74 kati ya 430 vilivyotembelewa, hasa kutokana na mawakala wengi wa chama, ambao walikuwepo katika vituo 429 kati ya 430 vilivyotembelewa. Waangalizi wa umma walikuwepo katika vituo 189 kati ya 430 vilivyotembelewa. Kwa ujumla, waangalizi wa EU walitathmini mwenendo wa upigaji kura kama "nzuri" au "nzuri sana" katika vituo 399 kati ya 430 vilivyotembelewa.

Zaidi ya nusu ya vituo vilivyotembelewa wakati wa kufunga havikufunga kwa wakati, hasa kutokana na kuchelewa kwa ufunguzi na wapiga kura wakiendelea kusubiri kwenye foleni kupiga kura. Kutofuata baadhi ya ukaguzi wa uadilifu unaohitajika wakati wa upatanisho wa kura, kama vile kutohesabu kura ambazo hazijatumika zilibainishwa katika vituo 9 kati ya 40 vilivyotembelewa kwa ajili ya kuhesabiwa, na kutozipakia katika bahasha zisizoguswa katika vituo10 kati ya hizi. Hatua hizi za usalama zimewekwa kuzuia uwezekano wa kuvurugwa. Lakini shughuli ya kuhesabu ilifanyika kwa njia ya uwazi, ingawa polepole, na sio kila wakati kulingana na sheria. Hakuna malalamiko rasmi, hata hivyo, yaliyowasilishwa katika vituo vilivyotembelewa. Fomu za matokeo ya kinyang'anyiro cha urais hazikuonyeshwa maramoja katika nusu ya vituo vilivyotembelewa, na hivyo kuathiri uwazi.

Kufikia tarehe 10 Agosti, timu za EU EOM zilikuwa zimefanya uchunguzi 192 katika Vituo vya Kujumlisha Maeneo Bunge (CTC). Katika kesi 13, kulikuwa na watu wasioidhinishwa ndani ya CTC; waliovuruga kazi za wafanyakazi wa CTC katika kesi nne. Katika uchunguzi 151, bahasha zote za usalama zilifika zikiwa salama. Waangalizi wa EU, hata hivyo, walibaini kutoweza kutazama mchakato huo katika kesi 11 kwa sababu ya umbali kutoka kwa meza. Katika uchunguzi 7 kati ya 192 hakuna mawakala wa chama walikuwepo. Ujumlishaji wa kura bado unaendelea.

**Utatuzi wa Migogoro ya Uchaguzi**

Mfumo wa kisheria hutoa upatikanaji wa suluhisho la kisheria linalofaa. Kwa ujumla kuna kiwango cha juu cha imani ya umma kwa mahakama. Mizozo ya kabla ya uchaguzi ilishughulikiwa kwa haraka na IEBC, Mahakama ya Mizozo ya Vyama vya Kisiasa (PPDT) na mahakama. Kutokuwepo kwa vikomo vya muda kwa rufaa za mahakama kulimaanisha kwamba zilikuwa zikiendelea katika mchakato mzima. Baadhi ya makataa ya usajili wa wagombea yalipungua ndani ya miezi miwili ya uchaguzi, na kusababisha idadi ndogo ya rufaa kuendelea hadi uchaguzi, na kusababisha sintofahamu, na kuhatarisha uendeshaji wa uchaguzi kwa wakati.

Usuluhishi wa migogoro ya uchaguzi unadhibitiwa sana, na taratibu zilizofafanuliwa vyema, ambazo zimefanya kazi kwa ufanisi hadi sasa. Wagombea waliogombea waliwasilisha migogoro 199 dhidi ya vyama kwenye uteuzi, ambayo iliamuliwa na PPDT. Kesi zilishughulikiwa ndani ya mwezi mmoja, kama inavyotakiwa na sheria, kwa kuwezeshwa na washiriki 18 wa ziada wa mahakama ya dharura. PPDT ilikuwa rahisi kufikiwa, na kugatua maeneo saba kitaifa, na kufungua na kusikilizwa kwa kesi kielektroniki. Mizozo inayohusiana na usajili wa wagombea ilisimamiwa na Kamati ya Kusuluhisha Mizozo ya IEBC (DRC). Kwa mchakato huu, kesi 325 zililetwa kwa kamati, ambazo zote zilisikilizwa na kuamuliwa ndani ya muda uliowekwa wa siku 10. Maamuzi 42 kati ya haya yalikatiwa rufaa katika Mahakama Kuu.

Kulikuwa na juhudi za pamoja na zilizofaulu za mahakama kushughulikia mizozo ya uchaguzi kwa haraka. Licha ya hayo, kukosekana kwa makataa ya kukata rufaa kutoka DRC kulisababisha kesi kuendelea hadi siku za kukaribia uchaguzi, na hivyo kuleta sintofahamu kwa maandalizi ya IEBC. Malalamiko ya kikatiba ya kupinga uhalali wa maamuzi ya IEBC kuhusu vipengele kadhaa vya taratibu za uchaguzi yaliendelea mbele ya mahakama hadi tarehe 8 Agosti. Masomo hayo yalihusu utawala, ikiwa ni pamoja na nyakati za upigaji kura kutoka kwa wakenya wanaoishia nchi nza kigeni, hadi ukiukaji wa sheria unaotarajiwa katika kushindwa kwa sajili ya wapigakura katika vituo vya kupigia kura.

Mfumo wa kieletroniki wa Taarifa hii ya Awali unapatikana kwenye tovuti wa www.eomkenya2022.eu. Kwa taarifa zaidi tunakuomba uwasiliane na:

Marek Mracka, Afisa wa Habari EU EOM, simu. +254 712 070 907,
marek.mracka@eomkenya2022.eu

**Ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi wa Umoja wa Ulaya**
*Sankara Hotel – 05 Woodvale Grove*
*Westlands, Nairobi, Kenya*